

Utafiti wa wakulima wa nje wa miwa Kilombero

Taarifa ya Mrejesho wa Wadau

Mei 2015

Andiko hili ni muhtasari wa utafiti uliofanywa na watafiti kati ya mwaka 2013 na 2014 juu ya wakulima wa nje wa miwa na kipato chao katika maeneo yaliyo karibu na Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Tanzania. Hili andiko linakusudia kutoa mrejesho kwa wahojiwa na watu wengine wanaopenda kujua masuala haya, pamoja na wadau wengine na kutoa fursa ya kupashana habari, kutoa malalamiko ya washiriki, na kuwasilisha matokeo ya utafiti na mapendekezo yetu.

Kuhusu utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Bwana Emmanuel Sulle wa Chuo Kikuu cha Western Cape, Afrika Kusini, akisaidiwa na Bi Rebecca Smalley, mtafiti wa kujitegemea kutoka Uingereza. Malengo ya utafiti yalikuwa: (1) kuelewa jinsi Kampuni ya Sukari ya Kilombero na mpango wa wakulima wa nje unavyo fanya kazi; (2) kutathmini athari (chanya na

hasi) ya mpango huo katika eneo hilo; na (3) kutathmini jinsi biashara ilivyo athiriwa na ubinafsishaji wa mwaka 1998 na mambo mengine. Tulifanya mahojiano zaidi ya 50 kati ya mwezi Novemba na Desemba 2013 na wakazi wa vijiji vya Msolwa Ujamaa, Sanje na Signali. Vijiji vya Msolwa Ujamaa na Sanje vilichaguliwa kwa sababu vilikuwa na idadi kubwa ya wakulima wa nje na vyama vyao vya ushirika, na walikuwa hawajatembelewa na watafiti siku za hivi karibuni. Signali ilichaguliwa kama mfano wa kijiji nje ya eneo linalolimwa miwa. Pia tulifanya mahojiano 33 kipindi chote kati ya 2013 na 2014 na wadau kama vile vyama vya ushirika vya miwa, kampuni, Bodi ya Sukari Tanzania na viongozi wa serikali. Taarifa ya kina ya utafiti huu imechapishwa tofauti na inapatikana katika tovuti hii: http://www.plaas.org.za/plaas-publication/FAC_WP106_Tanzania_sugar

Pia muhtasari wake unapatikana katika tovuti hii: <http://www.plaas.org.za/plaas-publication/Tanzania-Ksugar-FAC>

Historia

Vijiji katika sehemu hii ya Bonde la Kilombero vilikua na kubadilika kwenye karne ya ishirini wakati walowezi walipowasili kupitia mpango wa vijiji vya ujamaa na kufanya kazi katika kampuni ya sukari, reli ya TAZARA na biashara. Kwa asili yao, wakazi katika eneo hili walilima mtama, mpunga, mahindi, ndizi na mbogamboga. Watu wa Signali, walivua samaki katika Mto Kilombero. Hivi sasa, Kampuni ya Sukari ya Kilombero, ni mzalishaji mkubwa wa sukari nchini Tanzania.



Kielelezo 1. Ramani inayoonyesha mahali ilipo Kamapuni ya Sukari ya Kilombero pamoja na mikoa muhimu ambapo uhamiaji wa kiuchumi hutokea kuelekea kwenye eneo lililofanyiwa utafiti

Miaka ya 1920

- Wahindi walileta zao la sukari Tanzania

1960

- Kampuni ya Sukari Kilombero ilianzishwa chini ya ufadhili wa benki za nje ya nchi na mashirika ya maendeleo. Ikaanza na shamba lenye ekari 1,700 na kiwanda cha K1.
- Mpango wa makazi ulianzishwa katika maeneo ya Sonjo, Ichonde na Kichangani ambapo wakulima walizalisha miwa katika mfumo wa wakulima wa nje
- Vikundi vidogo vya wakulima pia vilizalisha miwa

1967

- Kampuni ya Sukari ya Kilombero ilitaifishwa kufuatia Azimio la Arusha, na serikali ya Tanzania ilitaka kujitosheleza katika uzalishaji wa sukari.

Miaka ya 1970

- Miwa ilianza kulimwa katika mashamba ya vijiji vya *Ujamaa*

1974

- Kampuni ya Sukari ya Kilombero ilianzisha shamba la pili na kiwanda cha K2, kaskazini mwa Kidatu. Mradi huu ulifadhiliwa na Benki ya Dunia na serikali za Uholanzi na Denmark.

1976

- Kiwanda cha K2 kinaanza kukamua miwa.


1998

- Serikali inabinafsisha Kampuni ya Sukari ya Kilombero, wamiliki wapya wanaongeza uzalishaji wa miwa, wanafufua uwezo wa kiwanda, wanaboresha miundo mbinu na kuboresha mfumo wa malipo kwa wakulima wa nje.

2001

- Kampuni ya Sukari ya Kilombero inajenga daraja la Mto Ruaha Mkuu

Umiliki wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero mnamo 1998 baada ya ubinafsishaji



Miradi miwili ya kuendeleza uzalishaji wa sukari Tanzania

- Katika programu ya Matokeo Makubwa Sasa (“Big Results Now”), serikali inataka kuongeza uzalishaji wa sukari. Serikali imeahidi kushirikiana na wawekezaji binafsi kuongeza mashamba makubwa ya miwa.
- Na katika mradi mwingine uitwao “Southern Agricultural Growth Corridor”, au SAGCOT, serikali ina mpango kwa ajili ya wawekezaji binafsi kuanzisha na kupanua mashamba ya miwa na mpango wa wakulima wa nje katika Kijiji cha Ruipa, karibu na Ifakara.

Hivi sasa, hairuhusiwi kwa makampuni mengine kujenga kiwanda cha miwa ndani ya eneo la km 40 za eneo la Kampuni ya Sukari Kilombero iliyopo Kidatu.

Matokeo makuu ya utafiti

Upanuzi

Idadi ya wakulima wa nje na mashambaya miwa iliongezeka sana baada ya ubinafsishaji mwaka 1998. Wakazi katika maeneo ya K1 na K2 walihamasishwa na kampuni, viongozi wa serikali za mitaa na serikali kuu na wanakijiji wenzao kulima miwa.

Viwanda hivi hufungwa katika kipindi Machi hadi Mei kwa ajili ya matengenezo na kwa sababu pia haiwezekani kuvuna miwa wakati wa msimu wa mvua nyingi.

Katika msimu wa 2013/14, kiwanda cha K2 kilikumbwa na matatizo ya umeme, na matengenezo yake yaliathiri kwa kiasi kikubwa kiwango cha miwa ya wakulima wa nje ambayo ilihitaji kukamuliwa.

Kampuni ya Sukari ya Kilombero

wakulima wa nje **8,500**

wanazalisha **43%** ya miwa inayokamuliwa na viwanda vya K1 na K2

K1 kinaweza kukamua tani 120 ya miwa kwa saa

K2 kina uwezo wa kukamua tani 150 kwa saa

Manufaa ya upanuzi

Upanuzi wa mpango wa wakulima wa nje tangu mwaka 1988 uliziwezesha kaya nyingi zaidi kufaidika na mapato ya miwa.

Ukuaji wa shughuli za miwa pia umechochea biashara katika miji midogo kama Ruaha na Kidatu. Mtu mmoja alisema, "Tazama jinsi watu wa Ruaha wanavyojishughulisha, ni kwa sababu ya Illovo".

Wakulima wametumia malipo ya miwa kujenga nyumba bora, kulimia mazao mengine na kusomesha watoto wao. Tulipowauliza wakulima wa nje jinsi gani wanatumia mapato yanayotokana na miwa, majibu waliyotoa mara nyingi ni ada ya shule ya sekondari kwa watoto wao.

Vipaumbele vya wakulima wa nje katika kutumia malipo yao ya miwa

- 1 Ada za Shule
- 2 Maboresho ya nyumba au kujenga nyumba mpya
- 3 Gharama za kilimo
- 4 Chakula na mahitaji mengine ya msingi ya kaya
- 5 Kununua au kukodisha ardhi
- 6 Malipo ya mikopo
- 7 Kusaidia ndugu katika familia kwa ujumla

Matatizo ya upanuzi

Tulizungumza na wakazi kadhaa ambao wangependa kujiunga na mpango wa wakulima wa nje lakini hawakuweza kumudu kununua au kukodi mashamba ya miwa. Mwanamke mmoja alituambia yeye anayajua matatizo ya sasa ya miwa lakini itakuwa muhimu kubahatisha: "Inakatisha tamaa, ila ni kama karata, kuna kupata au kukosa."

Tatizo moja linalosababishwa na upanuzi wa kilimo cha miwa ni kuongezeka kwa uhaba wa ardhi na kuwa ya ghali zaidi. Miwa imechukua nafasi ya mazao ya chakula katika mashamba mengi. Imekuwa vigumu kwa vijana, watu maskini na wageni kupata ardhi. Watu wanajenga nyumba katika milima kwa sababu hakuna nafasi tena vijijini. Gharama ya kukodi ekari moja ya ardhi ya kilimo Msolwa Ujamaa au Sanje ni kati ya shilingi 50,000 hadi 200,000 kwa mwaka na kati ya shilingi 700,000 hadi 1,500,000 kwa kununua. Ardhi ni nafuu kukodi katika maeneo yaliyo mbali kule chini bondeni. Huko Signali, gharama ya kukodisha ekari moja ya kulima mpunga ni kati ya shilingi 30,000 na shilingi 100,000 kwa msimu. Viongozi wa Signali walisema kuwa nao wameanza kukumbana na changamoto ya masuala ya ardhi huko pia.

Kwa sababu ardhi katika eneo la mashamba ya miwa imekuwa adimu na kwa sababu inaweza kuwa vigumu kwa ajili ya kulima mazao mengine karibu na mashamba ya miwa, wakazi wengi wamenunua au kukodi mashamba katika vijiji mbali mbali kama vile Signali au Lungongole kwa ajili ya kulima mahindi au mpunga. Hii inaweza kuwa njia nzuri kwa ajili ya familia kujiongezea kipato chao. Lakini wakati watoto wanapoachwa peke yao nyumbani kwa muda mrefu wakati wazazi wao wakiwa mbali mashambani, watoto (hasa mabinti (wasichana)) huwa katika mazingira magumu na wanaweza kuanza utoro shuleni. Tatizo hili huathiri wakulima maskini ambao wana fedha kidogo kwa ajili ya matrekta au wafanyakazi na ni lazima kutumia muda zaidi wa wiki kupanda, kupalilia na kuvuna.

Changamoto za wakulima wa nje

Kwa mujibu wa utafiti wetu, hali ya wakulima wa nje wa Kilombero imekuwa mbaya katika miaka ya hivi karibuni. Tatizo kubwa kwa wakulima wa nje ni kiwango cha chini cha sukari kwenye miwa yao.

Kiwango cha sukari

Kampuni inatarajia kuwa, wakulima watafikisha asilimia 10 ya kiwango cha sukari ili kupata bei nzuri, lakini watu waliohojiwa walisema wamekuwa wakirekodi kwa wastani asilimia 7.5. Kiwango cha sukari kinaweza kuathiriwa na:

- ugonjwa wa ukungu (smut disease)
- wadudu aina ya "whitescale"
- kuchelewa kati ya kuunguza na kukamua miwa,
- miwa kuvunwa wakati wa msimu wa mvua chache, na
- miwa kuvunwa mapema mno baada ya kupanda, kabla ya kukomaa.

"Wakulima wa nje wanaonekana kukosa ushauri au kufikiwa na maafisa ugani."

Hata hivyo, wakulima wa nje pia wanaamini kwamba mfumo wa upimaji wa kiwango cha sukari unathiriwa na rushwa na kukosa usahihi wa kipimo. Kuna ukosefu mkubwa wa uaminifu na uwazi katika upimaji wa kiwango cha sukari, lakini pia katika upimaji wa uzito wa miwa iliyovunwa na katika kuhesabu malipo ya wakulima.

Kati ya wakulima wa nje tuliowahoji, hakuna hata mmoja aliyekuwa ameuona Mkataba wa Ugavi wa Miwa ambao chama chao na kampuni zimetiliana saina. Pia, Mkataba wa Ugavi wa Miwa umeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na ni vigumu kuelewa vipengele mbalimbali. SACGA imetoa tafsiri ya Kiswahili ya mkataba huo, lakini washirika wengine walisema walikuwa wameomba tafsiri na walikuwa bado wanasubiri. Aidha, 'hati za malipo' za wakulima wa nje hazipo wazi sana. Haishangazi kuona wakulima kadhaa wakiwa hawana uhakika wa kimkataba na masuala ya uendeshaji kwa kina.

Matatizo 10 ya kawaida yanayo wasibu wakulima wa nje na ushirika wao

1	Kiwango cha chini cha <i>sukari</i> katika miwa
2	Mifumo ya upimaji uzito, kipimo cha kiwango cha <i>sukari</i> na hesabu za malipo si ya wazi au ya haki, na wakulima wa nje hawana uwakilishi
3	Ugumu katika kupata ardhi na mlolongo wa matatizo ya ukosefu wa mazao ya chakula na kulima mbali na nyumbani
4	Mbolea na dawa za kuua wadudu ni hafifu, ghali au hutolewa kwa kuchelewa mno
5	Kucheleweshwa kwa malipo ya miwa
6	Uwezo wa chini au uhakika wa viwanda
7	Hali ya mvua kuathiri udongo na barabara
8	Serikali kuruhusu uagizaji wa sukari kwa kiwango kikubwa
9	Rushwa au kukosekana kwa mfumo mzuri wa uvunaji wa miwa
10	Makato mengi mno (na yasiyo wazi).

Mkulima mmoja mdogo alisema, *“Hatuna uhakika sana ni jinsi gani malipo ya miwa hufanya kazi, kwa sababu hakuna mtu anayetuwakilisha katika shughuli ya kampuni hii, kwa mfano katika mizani, kupima kiwango cha sukari au kuhesabu “rendement.”*”

Baadhi ya wakulima walitueliza sisi kuhusu wakulima wa nje katika nchi nyingine.


Uvunaji

Uvunaji ni suala jingine linaloleta shida. Baadhi ya wakulima miwa yao huvunwa kwa kuchelewa sana katika msimu. Miwa ya wakulima wengine haivunwi kabisa. Kampuni inakadiriya ya kwamba katika msimu wa 2012/13, tani 65,000 ya miwa ya wakulima wa nje haikukamuliwa kabisa. Wakulima walisema kuwa vyama vyao na makandarasi hawafuati ratiba ya kuvuna, hivyo uvunaji haufuati tena utaratibu au haki. Inaonekana kuwapo ukiukwaji wa mchakato wa uvunaji na ukosefu wa usimamizi na uhibitaji wa kiasi cha miwa kinachozalishwa na wakulima wa nje.

Sababu moja ni kwamba mvua kubwa na mafuriko husababisha wakandarasi kushindwa kuyafikia mashamba. Sio barabara zote zinafaa kwa ajili ya magari, hasa kama mashamba yalibadilishwa kutoka mashamba madogo madogo ya mpunga. Tatizo hili liliongezeka zaidi wakati kampuni ilipoongeza muda wa msimu hadi Machi. Kwa mujibu wa Mkataba wa Ugavi wa Miwa, malori ya makandarasi lazima yaidhinishwe kwamba yanafaa kutumika kabla ya kuanza kwa kila msimu. Lakini baadhi ya malori tuliyo yaona yalionekana ya zamani na kushindwa kupanda milima. Barabara kuu ya Ifakara, ambayo inasimamiwa na Wizara ya Ujenzi, ipo katika hali

mbaya katika baadhi ya maeneo. Katika siku zijazo, serikali za Uingereza, Marekani na Umoja wa Ulaya zitatia saina makubaliano ya kufadhili ujenzi wa km 56 ya barabara ya lami kati ya Kidatu na Kiberege na kati ya Signali na Kibaoni.

Sababu ya pili kwa nini uvunaji haupo kwenye mpangilio ni kwamba wakandarasi wakati mwingine wanalazimika kwenda kwenye mashamba ya miwa ambapo moto umelipuka. Kama moto utasambaa hadi kwenye shamba la mwanachama wa ushirika tofauti, husababisha matatizo zaidi. Baadhi ya mioto ni ajali, lakini wakati mwingine wakulima wakubwa hufanya makubaliano (dili) na viongozi wa vikundi au viongozi wa vyama kwa makusudi kuanza kuchoma moto kwenye mashamba madogo ambapo moto husambaa hadi kwenye mashamba yao wenyewe. Wamiliki wa makampuni ya mikataba mara nyingi pia wenyewe huwa na mashamba makubwa ya miwa, na ni muhimu kuwa na angalau ekari 50 ili kuchaguliwa kuwa kiongozi wa chama. Hii inatengeneza fursa kwa wasomi kuweza kudhibiti mchakato wa uvunaji na kushinikiza kwa maslahi ya wakulima wakubwa.



Mkataba wa ugavi wa miwa

Makundi mbalimbali ya wakulima yana mahitaji na changamoto tofautitofauti

Tuliona makundi matatu ya wakulima wa nje: wamiliki wa mashamba makubwa; wakulima wa kati wenye ekari za miwa kati ya 5-20; na wakulima wadogo wenye chini ya ekari 3 za miwa. Wakulima wa nje walio wadogo zaidi mara nyingi ndio wenye fedha kidogo na ndio walio katika hatari zaidi ya kuathirika na ucheleweshaji wa uvunaji. Wao wanaminywa sana na wakulima wakubwa, rushwa na upendeleo katika mfumo uliopo, kushuka kwa faida inayotokana na miwa, na ukweli kwamba idadi ya wakulima wa nje imeruhusiwa kukua zaidi ya uwezo wa kampuni wa kukamua miwa. Mpango wa wakulima wa KSCL ni mzuri kwa kuwa upo wazi kwa kila mtu, lakini wakulima wa nje na maskini hawalindwi na mfumo uliopo sasa. Hapo awali, wakulima wa nje walichukua hatua ili kuboresha hali yao kwa kuonyesha hadharani na kuanzisha vyama vya ushirika vya kuwakilisha maslahi yao. Chama kikubwa cha wakulima wa miwa cha KCGA, bado kinatoa asilimia 45 ya miwa yote inayozalishwa na

wakulima wa nje, lakini idadi ya vyama vya ushirika imeongezeka hadi kufikia 15. Kwa bahati mbaya, vyama hivi havishirikiani kila wakati juu ya masuala kama vile maboresho ya barabara. Pia wao huweka shinikizo kwa kampuni wapewe mgao mkubwa wa miwa na hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa tatizo la ziada la miwa isiyovunwa au kukamuliwa.

Kilimo cha pamoja kinaweza labda kutoa kinga kwa wakulima wa nje. Mfumo wa kilimo cha pamoja ni kazi iliyo katika mchakato. Matatizo ya urasimu, rushwa na marejesho hafifu kutoka kwa wanachama yameripotiwa.

Uagizaji wa Sukari kutoka nje ya nchi

Mbali na ucheleweshaji wa uvunaji, wakulima wa nje wanakabiliwa na ucheleweshaji wa malipo. Katika kipindi cha Agosti 2013, Kampuni ya Sukari ya Kilombero ilianza kuchelewesha malipo stahiki ya wakulima wa nje kwa mujibu wa miwa waliyowasilisha. Malipokwa wakandarasi yalisimamishwa na wakandarasi hawakuweza kuwalipa wakata miwa mishahara yao kamili.

Kampuni ilieleza kuwa ilikuwa na matatizo ya kifedha kwa sababu serikali iliagiza na kuingiza nchini sukari nyingi sana yenye bei nafuu. Hii ilimaanisha kuwa kampuni haikuweza kushindana katika soko na kuuza

sukari ya kutosha. Biashara ya sukari ya magendo na udhibiti dhaifu juu ya uagizaji wa sukari nchini ni tatizo la kudumu. Mwaka 2013, kampuni ilishusha bei ya miwa kutoka shilingi 69,000 kwa tani hadi shilingi 62,889 kwa tani. Kampuni ilidai kuwa uuzaji wa sukari uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na uingizaji holela wa sukari nafuu kutoka nje ya nchi. Katika msimu wa 2013/14, bei ikaanguka hadi shilingi 58,000 kwa tani. Afisa wa kampuni alituambia, "Sisi tupo katika hali ya dhiki kwa sababu ya uingizaji wa sukari." Afisa mwingine wa kampuni alisema kwamba wangependa kuongeza uwezo wa viwanda vya K1 na K2 lakini hawawezi kumudu katika soko la sasa.

Watu kadhaa tuliowahoji walilalamika kwamba makato yameongezeka hivi karibuni. Ndiyo, kwa mujibu wa utafiti wetu, tangu msimu wa 2008/09 gharama ya makato imeongezeka. Pia tuligundua kuwa bei ya miwa iliyolipwa kwa wakulima wa nje imeongezeka hivi karibuni, hivyo makato na bei vimeongezeka kwa kiwango fulani. Makato pekee ambayo yameongezeka zaidi kuliko mengine yote kwa bei ya miwa, ni gharama ya kukata miwa. Sisi tulilinganisha gharama za makato kwa KCGA, MUCGA na SACGA tukakuta sawa kabisa. Lakini, kiwango cha sukari na bei ya miwa imekuwa ikipingua, hivyo wakulima wanapata mapato ya chini kwa jumla kutokana na matumizi makubwa zaidi kwa makato.

Ulinganisho wa vyama vitatu vya wakulima wa nje			
	KCGA	MUCGA	SACGA
Mwaka ilipoanzishwa	1991	2008	2012
DRD (uwasilishaji wa miwa kwa kota)	Tani 800 kwa siku	Tani 233 kwa siku	Tani 63 kwa siku
Idadi ya wanachama	2,500	856	342
Ada ya kiingilio	Shilingi 3,000	Shilingi 12,000	Hakuna
Usafirishaji (hadi 10km)	Shilingi 6,380/tani	Shilingi 6,200/tani	Shilingi 6,300/tani
Usafirishaji (11–21km)	Shilingi 8,250/tani	Shilingi 8,000/tani	/
Ukataji wa Miwa	Shilingi 6,380/tani	Shilingi 6,200/tani	Shilingi 6,300/tani
Upakiaji	Shilingi 3,800/tani	Shilingi 3,330/tani	Shilingi 3,600/tani
Ada ya uanachama	Shilingi 300/tani	Shilingi 500/tani	Shilingi 500/tani
Huduma za jamii	Shilingi 200/tani	Shilingi 500/tani	Shilingi 300/tani
Ada ya TASGA	Shilingi 100/tani	/	/
Mchango wa shule ya sekondari	Shilingi 300/tani	/	/
Gharama za ofisi	/	/	Shilingi 200/tani
Mfuko wa mitambo	/	Shilingi 500/tani	
Mitambo iliyopo kwa huduma za uvunaji	Malori 2, greda 1 na mitambo 2 ya upakiaji	Mtambo 1 wa upakiaji	Hakuna

Malipo ya miwa

Kampuni ya Sukari Kilombero hutumia hesabu ngumu kupanga kiasi ambacho kila mkulima mdogo anapaswa kulipwa kwa tani. Mwanzoni mwa msimu, kampuni ilikubali bei ya muda ya miwa. Bei hii ilitokana na kiwango cha wastani cha sukari ambacho wakulima walitarajiwa kufikia katika msimu. Hatua hii inaitwa "rendement" na kwa kipindi cha misimu michache imekuwa 10%. Wakati mkulima apelekapo miwa yake, hupimwa kiwango cha sukari. Hiki kipimo hutumika kurekebisha bei kuwa ya juu au chini, na pia, kuamua ni kiasi gani mkulima atalipwa kwa tani mwezi unaofuata. Kama kiwango cha sukari ni kikubwa kuliko 10%, bei itaongezeka. Kama kiwango cha sukari ni chini ya 10%, bei itapungua. Hii inaitwa "relative rendement". Wakati kampuni inamlipa mkulima anapopeleka miwa yake, hubakiza 10% mpaka mwisho wa msimu. Mwishoni mwa msimu, kampuni huhesabu ni kiasi gani cha sukari na molasses kimeuzwa katika soko. Kama kiasi hicho kilikuwa zaidi kuliko ilivyotarajiwa, kampuni huongeza bei ya miwa. Kama iliua kidogo kuliko ilivyotarajiwa, kampuni itapunguza bei. Kisha inamlipa mkulima 10% ya malipo yake yaliyobaki, ambayo hurekebishwa kama bei imepanda au kushuka.

Maisha katika Bonde la Kilombero

Ardhi na vipato

Wanavijiji wote tuliowahoji, katika siku za nyuma wamekuwa wakishiriki katika kilimo cha miwa kama wanachama, wakulima wanaofanya kazi, au wamiliki ambao huajiri vibarua. Soko kwa ajili ya kukodisha ardhi limekuwa muhimu sana katika eneo hilo. Wakulima wengi wa nje hutumia ardhi waliyorithi au ardhi walizogawiwa na serikali ya vijiji vyao kwa ajili ya miwa, na kisha kununua au kukodi ardhi ya ziada kwa ajili ya kulima mpunga au mahindi. Kwa wastani, wakulima wa nje wa Msolwa Ujamaa na Sanje humiliki au kukodi ekari 15.5 kwa ujumla kwa miwa, mpunga na mahindi. Watu watatu tuliowahoji walituambia hawakuweza kumudu kuwa wakulima wa nje. Kwa wastani, watu wale walikuwa na mashamba ya ekari 1.8 ya mpunga au mahindi tu. Wakazi wa Kijiji cha Signali hawakuweza kulima miwa kwa kuwa wako mbali na kampuni ya miwa, na watu watano tuliozungumza nao walikuwa na wastani wa ekari 10 za mpunga na mahindi. Hii inaweza kuonyesha kwamba wakulima wa miwa wa nje wana ardhi zaidi na hujiona kuwa bora zaidi kuliko wakulima wasiolima miwa.

Tulikutana na watu wawili tu kwenye vijiji vya Msolwa Ujamaa na Sanje ambao wanafanya kazi kwenye kampuni. Wanakijiji walisema kampuni inatoa zaidi ajira za kipato cha chini, kazi za muda mfupi kama vile kupalilia au ukataji wa miwa na kuwa wafanyakazi wengi huja kutoka nje ya eneo hilo.

Wakulima wengi huajiri vibarua kwa ajili ya mashamba yao na kuuza angalau baadhi ya mahindi au mchele wanaouzalisha pindi wanapohitaji fedha. Wakulima maskini mara nyingi huajiri vibarua kwa sababu ya kukosa muda au afya nzuri ya kufanya kazi zote wenyewe.

Vyanzo vingine vya mapato

Vyanzo vya kawaida vya mapato



Kuuza vyakula, maziwa na mazao mengine ya kilimo



Mapato ya biashara ya duka



Kuuza pombe za asili



Kazi ya kibarua

Vyanzo visivyo vya kawaida



Kufanya kazi hospitalini




Kazi ya upishi



Kufanya kazi katika ofisi ya kijiji



Mwalimu



Matrekta hutumiwa na wakulima katika maeneo yanayolima miwa hasa kwa kung'oa na kupanda tena miwa mwishoni mwa msimu wake. Lakini kwa ujumla, upatikanaji wa matrekta unaonekana kuwa mgumu na ghali. Kuna matumizi makubwa ya matrekta na ng'ombe ambayo wakulima wadogo hufanya katika maeneo yanayozalisha mpunga. Katika maeneo ya Signali, matrekta yapo tayari kwa watu binafsi kukodisha kwa kati ya shilingi 40,000 hadi 60,000 kwa ekari na dereva.

Matatizo ya kifedha

Kwa sababu ya matatizo yaliyojadiliwa katika taarifa hii, wakulima wa nje wanapambana na ucheleweshwaji wa malipo au malipo ya chini kuliko wakulima hawa walivyotarajia. Baadhi yao wanapata hasara kutokana na ulimaji wa miwa. Katika kukabiliana na hasara hizi, wakulima huchukua mikopo na kujaribu kutafuta fedha kwa njia nyingine au kupunguza matumizi.

“Sisi tunashindwa kutunza familia zetu,” alisema mkulima mmoja mdogo wa nje.

Baadhi ya wakulima wa nje hufikiria kujiondoa kulima miwa. Wengine wanaweza kulazimika kujiondoa kwa sababu ya madeni.

Mwanamke mmoja katika kijiji cha Msolwa Ujamaa alitumbua,

“Sisi tunafanya kila kitu katika mashamba yetu kwa gharama ya shilingi milioni 1 kwa ekari. Hili linaweza kutuletea mapato ya shilingi 1,500,000. Hiki ni kipato cha chini sana. Sisi tunahisi kuchoka, na labda tatalazimika kuacha kulima miwa.”

Lakini uamuzi wa kuachana na kilimo cha miwa na badala yake kulima mpunga au mahindi si rahisi. Wakulima wa nje hutegemea malipo ya miwa na matumaini yao ni kwamba mambo yatakuwa bora. Inaweza kuwa ghali kung'oa miwa, kuipanda upya na kutumia dawa. Wakulima wanapotaka kubadili mazao mengine, huhofia wadudu waharibifu na ndege kutoka katika mashamba ya miwa. Pia, mahindi na mpunga huwa na kazi kubwa zaidi kuliko miwa na huwa katika hatari kubwa ya kuharibiwa na mafuriko na ukame.

Wakati wa utafiti wetu, bei ambayo wakulima walipokea kwa gunia moja la mchele ilishuka kutoka shilingi 100,000

hadi shilingi 40,000 na kupanda tena hadi shilingi 50,000. Katika maeneo ya Signali, ambapo miwa hailimwi, bei ya chini ya mchele iliathiri kwa kiasi kikubwa kipato cha kaya. Wakazi wa Signali walisema wanauza magunia mengi zaidi ya mchele ili kufidia gharama ya kilimo cha mpunga, na kuhifadhi kiasi kidogo sana cha mchele majumbani kwa ajili ya matumizi ya chakula. Wakulima walipunguza matumizi kwa kutolima mashamba yao yote, kwa kutumia vibarua wa bei ya chini na kupunguza manunuzi. Wakulima maskini wa mpunga wanakosa malipo ya fedha zinazotokana na miwa na kwa sababu wanalazimika kuuza baadhi ya mazao yao ya chakula kwa ajili ya fedha, kaya zao zinaweza kukabiliwa na uhaba wa chakula.

Katika eneo hili ni vigumu watu kupata mikopo. Kwa sababu ya ucheleweshwaji wa malipo na faida inayotokana na miwa kuanguka, baadhi ya wakulima wa nje hukodisha mashamba yao ya miwa kwa watu wengine kwa sababu wanahitaji fedha kwa haraka. Tunaamini kwamba kama changamoto za sasa za fedha zitaendelea, watu zaidi wanaweza kulazimika kuuza au kukodisha mashamba yao kwa wengine katika maeneo yanayolima miwa na katika maeneo kama vile Signali.

Hitimisho na mapendekezo

Baada ya ubinafsishaji mwaka 1998, kampuni ilifanya mabadiliko ya kuboresha uzalishaji wa miwa na miundombinu ya usindikaji na mfumo wa malipo kwa wakulima wa nje. Ilitoa jukumu kubwa kwa vyama vya wakulima na wakandarasi wa ndani, na kuchangisha fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya mafunzo. Kwa kupitia upanuzi, wakulima zaidi katika eneo linalolima miwa wamekuwa ni wakulima wa nje na hunufaika kutokana na malipo ya miwa. Hata hivyo, tunaamini kwamba mpango wa upanuzi haukufanyika kwa umakini wa kutosha na kampuni imeshindwa kuhakikisha kwamba viwanda yake vinaweza kuvuna na kukamua miwa yote inayozalishwa na wakulima wa nje. Hakuna uangalizi wa kutosha katika uvunaji, upakiaji, usafirishaji na upakuaji. Pia hakuna mwongozo wa kutosha unaotolewa kuwasaidia wakulima wa nje kuinua viwango vya sukari na kutoa usimamizi wa mazao. Madai ya rushwa na upendeleo ndani ya mfumo yameongezeka. Tunaamini serikali ya Tanzania inaweza kufanya mengi zaidi ili kusaidia wakulima wa nje na kudhibiti uingizaji wa sukari kutoka nje ya nchi. Pamoja na kwamba serikali ilikuwa na moyo wa kuongeza uzalishaji wa miwa, ilishindwa kupanga vizuri kwa ajili ya shinikizo lisiloepukika juu ya mahitaji ya ardhi ambayo yangeweza kusababisha kuongeza upanuzi wa eneo la kilimo cha miwa na utitiri wa wafanyakazi na wafanyabiashara katika maeneo hayo. Mwisho, tuliona kwamba kilimo cha mpunga ni shughuli muhimu kwa wakazi katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na wakulima wa nje.

Wakulima maskini na wakazi katika maeneo yanayozalisha mpunga kama vile Signali wanateseka kutokana na kushuka kwa bei ya soko la mchele.

Wakati wa utafiti, tulisikia mapendekezo mengi kwa ajili ya maboresho. Tumezingatia mawazo hayo na uchambuzi wetu wenyewe na kutoa mapendekezo yafuatayo kwa ajili ya mabadiliko:

Matatizo makuu kama yalivyoainishwa katika utafiti wetu

1	Ukosefu wa usimamizi na udhibiti katika upandaji, uvunaji na utoaji wa miwa.
2	Upanuzi usiodhibitiwa wa eneo la wakulima wa nje, na tatizo linalohusiana na udogo, na ugumu wa upatikanaji wa mashamba.
3	Ukosefu wa msaada kwa ajili ya wakulima wadogo wa nje.
4	Huduma isiyotosheleza ya ugani kwa ajili ya wakulima wa miwa wa nje lakini pia wakulima wa mpunga na mahindi.
5	Kukosekana uaminifu wakati wa upimaji wa uzito wa miwa.
6	Uhaba wa ardhi na kipato cha chini huhamasisha wakulima kulima mashamba mbali na nyumbani na kuwaacha watoto wakiwa nyumbani peke yao.
7	Rushwa na upendeleo katika mfumo wa wakulima wa nje, ni mzigo kwa wakulima wadogo na masikini.
8	Upatikanaji usioridhisha wa pembejeo na mikopo.
9	Utawala mbovu na usimamizi duni wa uagizaji wa sukari wa kitaifa.
10	Wakulima wanafikiri hawawezi kuachana na miwa kwa sababu ya gharama za kilimo cha mpunga na bei ya chini ya mchele, na hatari ya ndege, wadudu na mioto ya miwa.

- Bunge la Tanzania na Halmashauri za Wilaya na Vijiji zinapaswa kufanya kazi zaidi kufuatilia utendaji wa viongozi, kutoka ngazi ya kitaifa hadi ngazi ya kijiji. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba sheria za nchi katika sekta ya sukari zinatekelezwa.
- Utoaji wa huduma za ugani na mafunzo kwa wakulima wa nje yanapaswa kuongezwa. Kampuni, serikali na wafadhili wanapaswa kufanya kazi pamoja ili kuboresha maarifa ya wakulima kuhusu ugonjwa wa ukungu na kiwango cha *sukari*.
- Ushirika, kampuni na wanachama wa sekta nyingine wanapaswa kufanya kazi pamoja na kujenga mifumo bora ya kupima uzito wa miwa inayoletwa na wakulima wa nje, kupima kiwango cha sukari na kukokotoa hesabu za malipo. Kampuni inaweza kufanya utafiti wa kiwango cha sukari katika uendeshaji na kuchapisha matokeo, ili kurejesha imani ya wakulima wa nje kwa mfumo na kubaini sababu zinazosababisha matokeo duni.
- Mkataba wa Ugavi wa Miwa na hati za malipo za wakulima zinapaswa kuwa rahisi kueleweka. Mkataba wa Ugavi wa Miwa lazima kutafsiriwa kwa Kiswahili na kusambazwa kwa wakulima wa nje. Kampuni lazima iweke wazi kama wakulima wa nje wanapata faida kutokana na sukari, molasses, masalia na ethanol. Ushirika lazima uweeze wakulima wa nje matokeo ya kisheria kutokana na kiwanda kusitisha uzalishaji na uchelewashaji wa malipo.
- Ushirika, makandarasi na kampuni lazima wawajibike zaidi kwa wakulima wa nje. Adhabu mpya na motisha vinaweza kuwa vinahitajika ili kuhakikisha kwamba biashara ya sukari inafanyika kwa haki, kwa ufanisi na kwa uwazi. Kwa mfano:
 - Ushirika lazima uongeze uwezo wao wa kufanya mchakato wa ratiba na wajibu wao kwa ujumla kwa ajili ya kuwasilisha miwa ya wanachama wake. Ushirika lazima uajiri mameneja wenye sifa ya kuendesha sehemu ya uendeshaji wa majukumu yao.
 - Fikiria njia ya kuufanya uongozi wa ushirika kuwa wa uwakilishi zaidi wa wanachama wao, ikiwa ni pamoja na wakulima wa nje wa kike na wakulima wadogo wa nje.
 - Wakulima wa nje, kampuni na wadau wengine wa sekta lazima wajadili njia za kuzuia kuvurugika kwa ratiba ya uvunaji kutokana na mioto ya miwa na hongo.
 - Kampuni lazima itekeleze sheria za Mkataba wa Ugavi wa Miwa kuhusu hali ya malori ya usafirishaji.
 - Fikiria motisha au adhabu ili kuepuka ucheleweshaji katika utoaji na ukamuaji wa miwa.
 - Wafadhili kama vile EU wanapaswa kufuatilia kwa karibu miradi yao kama vile maboresho barabara na mashamba ya pamoja.
- Serikali na wafadhili wanapaswa kutoa mwongozo wa uwekezaji binafsi na wa umma wa kutosha chini ya usimamizi mkali na uwazi kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara, mifereji ya umwagiliaji na mifumo ya mifereji ya utoaji maji.
- Kampuni, wafadhili na wadau wa sekta wana haja ya kuboresha mipango, usimamizi na ufuatiliaji wa uzalishaji wa wakulima wa nje.

Kuna haja ya majadiliano yanayohusisha wakulima wa nje na wakazi wengine wa ndani juu ya hatma ya ulimaji wa nje wa miwa katika eneo hilo. Maeneo ya uwezekano wa kufanyia kazi:

- a) Kuchunguza matatizo ya mashamba ya bloku yaliyoripotiwa. Utafiti ufanyike kubaini kama kilimo cha mashamba ya bloku inaweza kuwa njia ya kuwasaidia wakulima wadogo na kulinda ushiriki wao katika mradi huu.
 - b) Kufanya mazungumzo juu ya ufumbuzi wa muda mrefu wa tatizo la uzalishaji wa ziada Kilombero. Ufumbuzi unaweza kuwa ni pamoja na kupunguza mgao wa ushirika na kuanzisha motisha, uhakika wa masuala na adhabu ili kuongeza ufanisi na uwezo wa viwanda vya kukamua miwa. Kutekeleza mipango ya kuongeza uelewa wa ndani juu ya hatari ya uzalishaji wa miwa wa nje na mpango wa kikanda kwa ajili ya maeneo yote ya miwa na mazao ya chakula katika maeneo ya ugavi. Kutoa mipango kwa wadau mbalimbali na msaada kwa ajili ya wakulima wadogo ambao wanataka kuachana na miwa na kupita katika mpito kwa mazao mengine, na kutekeleza hatua za kuimarisha uzalishaji mdogo wa mchele na mazao mengine ya chakula na masoko kwa ujumla zaidi, ikiwa ni pamoja na zaidi ya kanda za wakulima wa nje.
8. Serikali na wadau wa sekta ya sukari Tanzania lazima waboreshe mchakato kwa kutoa leseni na vibali vya kuagiza sukari. Wanapaswa kuchukua hatua kusaidia makampuni ya sukari kusimamia kuzorota kwa mzunguko wa fedha inayosababishwa na uingizaji wa sukari kutoka nje. Wanapaswa pia kuanzisha hatua ili kuepuka kuwatwisha gharama wakulima wa nje na makundi mengine yenye matatizo kama vile wakata miwa.
 9. Ili kusaidia kufikia malengo hapo juu, inaweza kuwa na manufaa kuandaa jukwaa kwa ajili ya wakulima wa nje, ushirika, kampuni na maafisa wa sekta hii kwa kukutana pamoja na kujadili changamoto na fursa. Itakuwa muhimu kuwaalika wawakilishi wa ushirika wa wakulima wa nje kutoka nchi nyingine katika Afrika ili kujadili jinsi miradi inavyofanya kazi na nini changamoto wanazokabiliana nazo.
 10. Zaidi ya miwa, kuna haja ya kupata msaada zaidi kwa kilimo cha mpunga na mahindi katika eneo hilo, kama vile barabara na hifadhi (maghala) bora. Wafadhili na vikundi vya wakulima kama vile MVIWATA wanapaswa kufanya kazi na viongozi wa ardhi na wawakilishi wa SAGCOT kwa kutambua mahitaji makubwa zaidi katika eneo hilo na mabadiliko ambayo yangeweza kuleta tofauti kubwa kwa maisha ya watu katika eneo hilo.

Kwa Maelezo zaidi wasiliana na:

Bwn. Emmanuel Sulle, esulle@plaas.org.za
PLAAS
Chuo Kikuu cha Western Cape
Private Bag X17
Bellville 7535, Afrika Kusini, Simu: +27 (0) 21 959 3733

Bi Rebecca Smalley, rebeccasmalley@gmail.com

Bodi ya Sukari Tanzania

Barabara ya Sokoine / Mtaa wa Ohio
S.L.P. 4355
Dar es Salaam, Tanzania, Simu: +255 22 2111523,
Nukushi: +255 22 2130598

Barua pepe: sbt@cats-net.com

SUGECO / Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine

S.L.P. 3000, Chuo Kikuu,
Morogoro -TANZANIA
Simu. + 255 23 2603511-4. Nukushi: + 255 23 2604651
Barua pepe: sua@suanet.ac.tz

Ripoti ya Utafiti juu ya Kupunguza Umaskini (REPOA) [(www.repoa.or.tz). 2012 Mabadiliko ya miundo ya shirika kwa Wakulima wa Miwa wa Nje katika Tanzania: Ripoti ya mwisho].

Shukrani

Watafiti wanapenda kumshukuru kila mtu ambaye alishiriki katika utafiti huu. Tunamshukuru sana Bwana Jumapili Chenga kwa kulitafsiri andiko hili katika lugha ya Kiswahili.

Unaweza kuwasiliana naye kwa barua pepe:
j2chenga@gmail.com; Simu: +255 754 604 896